ESSA
Education Sub Saharan Africa

DIRA YETU NA KWA NINI NI MUHIMU

Dira yetu iko wazi:

"Matokeo yaliyobadilishwa ya kielimu barani Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara"

Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na Mkakati wa Elimu wa Bara la Afrika uliweka mfumo ili kukabiliana na changamoto zinazoikabili Afrika katika elimu. Serikali za Afrika chini ya Jangwa la Sahara zinawekeza 5% au zaidi ya GNP kwenye elimu na hili linachagizwa na wengine ikiwa ni pamoja na fedha za maendeleo, kampuni na mashirika yasiyo ya kiserikali.

Tathmini ya utafiti, data na athari ni muhimu katika kutengeneza sera na machaguo sahihi kwa kila mtu anayewekeza katika sekta hii, inaimarika vilivyo. Na bado inasalia kuwa na ubora tofauti, inaweza kuwa vigumu kufikia na mara nyingi huwa haijakamilika.

Sababu moja ya kuamini kuna fursa ya kuongeza ufanisi wa matumizi na kuvutia mtaji wa ziada.

Vilevile, huku ongezeko kubwa la watu likiendelea, nchi nyingi za Afrika tayari zinakabiliwa na changamoto nyingi, ngumu na za kimfumo katika utoaji wa elimu ambayo jamii zao zinahitaji.

KWA MUKTADHA HUU TUNAAMINI KWAMBA:

"Upatikanaji wa elimu katika ngazi zote na kwa ubora na umuhimu wake utakuwa muhimu kuamua kama ukuaji wa idadi ya watu unachukuliwa kuwa fursa ya kawaida au tishio kubwa kwa Afrika na dunia nzima".

Tunataka kufanya kila kitu tunachoweza pamoja na kila mtu tunayefanya kazi naye ili kusaidia kutatua changamoto ya ukosefu wa ajira kwa vijana, hata miongoni mwa wahitimu, wakati huohuo kama waajiri wanakabiliwa na uhaba mkubwa wa ujuzi.

NINI KINAHITAJI KUTOKEA ILI KUFANIKISHA DIRA YETU?

Kwa muhtasari:

"Kujiunga, kufahamisha, kuhamasisha, kuzingatia na kuongeza athari kwa kila mtu anayewekeza katika elimu barani Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara."

Hatua yetu ya kuanzia imekuwa kuwasikiliza wanafunzi, walimu, jamii, serikali, wafanyabiashara, wasomi, mashirika yasiyo ya serikali, watoa misaada na wengine ndani na nje ya Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Masuala haya ni wazi na yanayojulikana na ya dharura.

Tangu kuanzishwa mwaka 2016, kwa msaada mkubwa kutoka kwa Asasi Robert Bosch, njia yetu ya kusaidia ilikuwa kuanza katika sekta ya Elimu ya Juu na kuzingatia mambo manne::

- Kuwa kiunganishi amilifu.
- Kuhamasisha na kusaidia maendeleo ya uwezo.
- Kuenga kituo cha maarifa cha "Kutegemewa" kuhusu Elimu katika kanda na;
- Kuendesha maarifa katika vitendo kupitia kazi yetu na ushirikiano wetu na mahusiano yetu.

MIFANO YA KAZI YETU

Mifano hii inaonyesha jinsi kila kipengele na jinsi tunavyofanya kazi inavyoweza kufanya tofauti ya vitendo..

DEMOGRAFIA ZA KITIVO

Watu bilioni zaidi na viwango vinavyoongezeka vya ushiriki inamaanisha ongezeko kubwa la kitivo kuhitajika, hata kwa matumizi bora ya teknolojia. Lakini ni ngapi, wapi, lini na nini kinahitajika kufanywa sasa ili kuepuka msiba unaowezekana wa mamilioni ya Waafrika na jamii zao katika kutimiza uwezo wao?

Ikihamasishwa na ESSA, Baraza la Kitaifa la Elimu ya Juu (NCTE) la Ghana, Chama cha Vyuo Vikuu vya Afrika (AAU), na Ofisi ya Idadi ya Watu (PRB), kwa usaidizi kutoka kwa Wakfu wa MasterCard, wanashiriki katika jaribio nchini Ghana ili kukabiliana na changamoto hii pamoja na kuzalisha zana za kupanga na rasilimali nyingine ili kuhamasisha msaada wa kukabiliana na changamoto hii ya dharura. Jaribio lenye mafanikio linatoa uwezekano wa kuigwa na kutumika kwa wingi kote katika kanda.

KUBADILI MUONEKANO NA UPATIKANAJI WA UTAFITI WA KIAFRIKA KUHUSU ELIMU

Kwa sasa ni vigumu kupata utafiti bora wa Kiafrika kuhusu mada maalum. Ni vigumu hata zaidi kwa watafiti Waafrika kuchapisha kazi zao na kufanikisha ufahamu na ushawishi. Tunataka kubadilisha hili..

Pamoja na Kituo cha REAL katika Chuo Kikuu cha Cambridge na usaidizi kutoka kwa watoa misaada wawili na Wakfu wa Jacobs tunafanya hivyo. Hatua ya kwanza imekuwa kuleta ushahidi wenye msingi wa utafiti uliofanywa na watafiti walioko barani Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara na kutengeneza hifadhidata inayopatikana wazi, tangamanifu na inayoweza kutafutwa. Hivi karibuni itapatikana kwenye tovuti za ESSA na Kituo cha REAL. Majibu tuliyopata kuhusu hili na kuhusu usaidizi wetu kutoka kwa kongamano za watafiti nchini Burkina Faso yamekuwa yenye kutia moyo sana..

KUJARIBU KITUO CHA ATHARI YA UFADHILI WA KIMASOMO

Ufadhili wa kimasomo ni sehemu muhimu katika kufanikisha SDG4. Utafiti na uzoefu wetu unaonyesha kwamba kuna fursa ya kuongeza athari ya matumizi ya sasa na pia ili Afrika izidishe mazoea ya kimataifa. Kuna uwezekano hii itahamasisha uwekezaji zaidi na pia kuboresha matokeo ya wote waliohusika.

ESSA imeanza kukusanya ushahidi uliopo, kutambua mazoea bora na kufanya uchambuzi wa kimataifa/wadau, ili kuunda rasilimali (k.m. KPIs za athari ya ufadhili wa kimasomo na rasilimali bora za dijitali) na kuwasiliana kwa lengo la kubadilisha majadiliano na kuongeza athari.

KUJENGA "KITUO CHA MAARIFA CHA KUTEGEMEWA

Kuna maarifa na data nyingi muhimu zilizopo. Lakini iko mbali sana na kufikiwa kwa urahisi. Tunachotaka kufanya ni "Kukusanya" yale muhimu (k.m. Utafiti wa Kiafrika kuhusu elimu) Kutengeneza yanayokosa (k.m rasilimali kuhusu mifumo fanisi zaidi ya ufadhili wa kimasomo). Kisha kupitia kitovu chetu cha kidijitali cha maarifa na shughuli halisi zinatoa jukwaa la "Kuwasiliana" na "Kuunganisha" wale wanaohitaji maarifa fulani na wale wanao na maarifa hayo na yanayopatikana.

TUNAVYOFANYA KAZI

Vijana Waafrika ni kitovu cha yote tunayoyafanya

Tangu mwanzo kabisa Waafrika na vijana Waafrika hasa, wamechochea mawazo yetu. Hatua yetu inayofuata itakuwa kutengeneza jopo la Vijana wa pan-Afrika.

Mtazamo wa hatua kwa hatua

Tukianzia na Elimu ya Juu na kufanyia kazi mada chache tunajenga kasi ili kuongeza athari zetu zaidi na kupanua ufikiaji wetu.

Ushirikiano Mkubwa

Tunajenga jamii zenye nia kama vile viongozi wa kielimu, watafiti na wafadhili na kuwasilisha thamani halisi kwa njia ya kuhusisha. Uzinduzi wa tovuti yetu kwa lugha ya Kiswahili, Kiingereza na Kifaransa ni mfano mmoja tu.

Mfumo wa Ushirikiano

Kuna kazi nzuri sana inayofanywa na wengine wanaoshiriki maono yetu na hatuoni haja ya kurudia. Afadhali tujifunze kutoka kwao na tuunganishe michango na rasilimali zetu..

Mtazamo wa athari kubwa

Machaguo na shughuli zetu zinaendeshwa na kile kitakachokuwa na athari kubwa zaidi. Tunajua kwamba rekodi yetu ya uwasilishaji itabainisha mafanikio na uendelevu wetu..

Mtazamo wa gharama nafuu

Wafuasi, washirika na wafadhili wetu wametuwezesha kuweka gharama za chini kupitia kuazima, kazi ya kujitolea na manufaa mengine wanayoleta.

WASHIRIKA AMBAO NI WAFADHILI WA KWANZA WA ESSA

Robert Bosch Stiftung

mastercard foundation

JACOBS FOUNDATION
Our Promise to Youth

Vipaumbele vyetu kwa 2018/19:

Tunapofikia mwaka wetu wa pili, vipaumbele vyetu ni:

- Kuwasilisha athari kubwa kutokana na kazi yetu ya sasa.
- Kujenga na kuwasilishaa OpenESSA jukwaa letu la rasilimali la dijitali na mshirika wetu, Taasisi ya Hasso-Plattner (HPI).
- Kuanzisha rasmi jopo la vijana wetu wa pan-Afrika na Mwenyekiti wake kujiunga na bodi ya ESSA.
- Kukamilisha kazi na kuchangisha pesa ili kupeleka kituo chetu cha Maarifa ambacho ni kichanga hadi hatua inayofuata.
- Pamoja na washirika wetu Chama cha Vyuo Vikuu Afrika na Jobs.ac.uk kuunda ubao wa kazi za kitaaluma wa pan-Afrika.
- Kazi yetu kuhusu Hali ya data ya kielimu na uwezo wa Sayansi ya Data barani Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara kuanzia uzinduzi hadi hatua ya majaribio.
- Kuanzisha mipango yetu ya kwanza ya maendeleo kwa viongozi wa elimu

MAWASILIANO:

- Olaf Hahn: olaf@essa-africa.org
- Tracy Hart: tracy@essa-africa.org
- www.essa-africa.org
- T: @ESSA_africa
- F: @EducationSubSaharanAfrica

ESSA
Education Sub Saharan Africa